الدعوة الإلكترونية

EDC

# SABEEL ACADEMY

Kwa kurahisisha elimu za kisheria

# Uislam

## HATUA KWA HATUA

### Kipindi (3)

# USAFI WA MUISLAMU

Jina la mwanafunzi ........................................................



2

# USAFI WA MUISLAMU

Allah amemuamrisha Muislamu kuusafisha moyo wake uondokane na maradhi ya nyoyo, kama: husda, kiburi na mfundo. Pia kuusafisha mwili wake uondokane na najisi na uchafu. Muislamu akifanya hayo, atastahiki kupata mapenzi ya Allah, kama Allah alivyosema kwamba: «Kwa yakini, Allah anawapenda wenye kutubu sana na anawapenda wenye kujitwaharisha». (Sura Albaqara, aya 222).

Maana ya twahara

Kujisafisha najisi

Hadathi

Natawadha vipi?

# USAFI WA MUISLAMU

## Maana ya Tohara

**Chimbuko la maana ya twahara ni usafi, unadhifu na umaridadi**

Allah Mtukufu amemuamrisha Muislamu kuusafisha mwili wake na moyo wake. Ausafishe moyo wake uepukane na vitu dhahiri vya haramu, vitu vibaya na vichafu. Pia ausafishe moyo wake uepukane na Shirki na maradhi ya nyoyo, kama: husda, kiburi na mfundo. Akifanya hayo, atastahiki kupata mapenzi yaAllah, kama Allah alivyosema kuwa: «Kwa yakini, Allah anawapenda wenye kutubu sana na anawapenda wenye kujitwaharisha». (Sura Albaqara, aya 222).



Na Allah ameamrisha kujitwaharisha kwa ajili ya swala, kwa sababu swala ni kukutana na kuzungumza na Allah Mtukufu. Ni suala linalofahamika kwamba mtu anajisafisha na kuvaa nguo zake nzuri sana ikiwa atakutana na mfalme au rais. Hali ikoje basi kwa mtu ambaye anakutana na mfalme wa wafalme aliyetakasika?

### *Ni ipi twahara inayotakiwa kwa ajili ya swala?*

Allah amemuamrisha Muislamu kujitwaharisha kisheria kwa maana maalum kwamba ni amri ya wajibu ikiwa anataka kusali au kushika msahafu au kutufu Alkaaba Tukufu. Pia amefanya Twahara kuwa ni jambo linalopendekezwa katika mazingira kadhaa. Miongoni mwa mazingira hayo ni kusoma Kur'ani bila ya kushika Msahafu, kuomba dua, kulala na mengineyo.

Inamlazimu Muislamu akitaka kusali ajitwaharishe na mambo mwawili:

1. Najisi
2. Hadathi



## Kujisafisha najisi

- **Najisi** ni vitu yakinifu ambavyo sheria imehukumu kwamba ni uchafu na kutuamrisha tujisafishe kwa ajili ya kufanya ibada.
- **Msingi** katika vitu vyote ni kufaa kutumika na ni twahara. Najisi ni jambo la kuzuka. Kwa hiyo, tukiwa na shaka ya twahara ya nguo, kwa mfano, na tusiwe na hakika ya kuwepo kwa najisi, msingi ni kwamba nguo hiyo ni twahara**.**
- **Na tukitaka** kusali ni wajibu kwetu kujitwaharisha Najisi katika mwili, nguo na eneo ambalo tunasali.

### Vitu najisi ni:

| | |
|---|---|
| 1 | Mkojo wa mwanadamu na kinyesi chake. |
| 2 | Damu. Na damu chache inasameheka. |
| 3 | Mkojo na kinyesi cha kila mnyama ambaye ni haramu kuliwa (Tazama uk. 224). |
| 4 | Mbwa na nguruwe. |
| 5 | Wanyama waliokufa. (Makusudio ni wanyama wote waliokufa, isipokuwa tu mnyama ambaye anafaa kuliwa, ikiwa amechinjwa kwa namna ya kisheria. Tazama uk. ……). Ama maiti ya mwanadamu, samaki na wadudu ni twahara. |

### Kujitwaharisha na najisi:

Katika kuisafisha najisi iliopo katika mwili au nguo au mahali au sehemu nyingine, inatosha Najisi yenyewe kuondoka katika sehemu paliponajisika kwa kutumia nyenzo yoyote ambayo usafishaji umefanyika; kwa kutumia maji au kitu kingine, kwa sababu sheria imeamrisha kuondoa Najisi, na katika kusafisha Najisi hiyo haikuweka idadi maalum isipokuwa tu katika Najisi ya mbwa . (Najisi ya mbwa ni ute wake, mkojo wake na kinyesi chake). Katika najisi hiyo, sheria imeweka sharti la kuosha mara saba, mojawapo ya mara hizo iwe kwa kutumia mchanga. Ama Najisi zilizobaki, inatosha kusafisha najisi yenyewe, na kubaki kwa rangi na harufu hakudhuru, kama Mtume, Allahswallalahu alayhi wasalam, alivyomuambia Swahaba mmoja mwanamke katika kusafisha damu ya Hedhi kwamba: «Inakutosha kuosha damu na wala athari yake haikudhuru». (Abudaud, Hadithi Na. 365).

## Taratibu za kustanji na kwenda haja

- Inapendekezwa mtu akiingia chooni atangulize mguu wake wa kushoto na kusema: **«Bismillah Allahuma Inniy Audhubika mina khubuth wal khabaaith»** (Kwa jina la Allah. Ewe Mola wangu, naomba kinga kwako unikinge na mashetani wa kiume na mashetani wa kike).
- Na akitoka chooni atangulize mguu wake wa kulia na kusema: **«Ghufraanaka»** (Naomba msamaha wako).
- Ni wajibu kwake kusitiri utupu wake usionwe na watu wakati wa kwenda haja.
- Ni haramu kwake kwenda haja katika mahali ambapo kwa kwenda kwake haja katika mahali hapo atawaudhi watu.
- Inatakikana kwake, ikiwa yupo eneo la wazi, kutokwenda haja katika shimo, kwa sababu ya uwezekano wa kuwepo humo wanyama ambao anaweza kuwakera na wao kumkera.
- Inatakikana kwake kutoelekea Kibla na kutokipa mgongo wakati wa kwenda kwake haja. Ama akiwa yupo eneo la wazi na hakuna ukuta unaomkinga, ni wajibu kwake kufanya hivyo, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, swallalahu alayhi wasalam, isemayo kwamba: «Mkienda haja, msikielekee Kibla na msikipe mgongo kwa kukojoa na kwenda haja kubwa». (Bukhari, Hadithi Na. 386, Muslim, Hadithi Na. 264).
- Ni wajibu kwake kujilinda ili nguo zake na mwili wake usije ukapatwa na kitu katika Najisi zinazo peperuka. Ni wajibu kwake kusafisha kitakachompata katika hayo.
- Akishamaliza kujisaidia, inakuwa lazima kwake kufanya moja kati ya mambo mawili:

**Ama**

kusafisha mahali pa mkojo au kinyesi kwenye mwili wake kwa maji (kustanji).

**Au**

kusafisha mahali hapo kwa taulo tatu za karatasi au mawe matatu na mfano wake katika vitu ambavyo vinasafisha mwili na kuutakasa uondokane na Najisi (kujisafisha kwa kutumia kitu kikavu = istijmar).

## Hadathi

- Hadathi ni wasifu wa hali inayompata mtu inayomzuia kufanya ibada kabla ya kujitwaharisha, na sio kitu kinachogusika, kama Najisi.
- Hadathi inamuondoka Muislamu akitawadha au akioga kwa maji yaliyo Twahara. Maji Twahara ni ambayo hayajachanganyika na Najisi na kuathiri rangi yake, ladha yake au harufu yake.

**Hadathi inagwanyika mafungu mawili:**

1. Hadathi inayomlazimu mtu kutawadha ili imuondoke. Tunaiita (Hadathi Ndogo).
2. Hadathi inayomlazimu Muislamu kuoga na kueneza maji mwili wake ili imuondoke asiwe nayo. Tunaiita (Hadathi Kubwa).



## Hadathi ndogo na kutawadha kwa sababu yake:

Twahara ya Muislamu itabatilika na kulazimika kutawadha kwa ajili ya kusali ikiwa litampata jambo moja kati ya vibatilishi vifuatavyo:

1. **Kukojoa na kwenda haja kubw**a, na kila kilichotoka katika sehemu ya mkojo na haja kubwa, kama vile hewa chafu. Allah amesema katika kutaja vitu vinavyotengua Udhu kwamba: «…au yeyote miongoni mwenu akitoka kukidhi haja kubwa». (Sura Annisaa, aya 43). Na Mtume, swallalahu alayhi wasalam, katika kumuelezea mtu aliyekuwa na shaka kuwa amepata Hadathi akiwa ndani ya swala, amesema kwamba: «Asiondoke (na kukatisha swala) mpaka asikie sauti au avute (harufu ya) hewa chafu». (Bukhari, Hadithi Na. 175. Muslim, Hadithi Na. 361).
2. **Kushika sehemu za siri kwa matamanio,** bila ya kuwepo kizuizi. Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mwenye kushika dhakari yake atawadhe». (Abudaud, Hadithi Na. 181).
3. **Kula nyama ya ngamia.** Mtume aliulizwa kwamba: “Je, tutawadhe kwa sababu ya nyama za ngamia? Alisema: Ndio”. (Muslim, Hadithi Na. 360)
4. Kupoteza fahamu kwa kulala au wazimu au kulewa.

# Udhu

Twahara na Udhu ni miongoni mwa amali bora sana na adhimu sana. Allah kwayo anafuta dhambi na makosa madamu mja amemtakasia nia Allah akitaraji malipo kutoka kwake. Mtume wa Allah, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Mja Muislamu anapotawadha; akaosha uso wake, inatoka usoni mwake pamoja maji kila dhambi aliyoiangalia kwa jicho lake. Akiosha mikono yake, inatoka mikononi mwake pamoja na maji kila dhambi iliyofanywa na mikono yake. Akiosha miguu yake, inatoka pamoja na maji kila aliyoifanya kwa kutumia miguu yake, hadi anatoka akiwa safi; hana dhambi». (Muslim, Hadithi Na. 244).

## Ninatawadha kwa namna gani na nitaondoaje Hadathi ndogo?

Muislamu akitaka kutawadha ni wajibu kwake kunuia kwa maana ya kuwa na kusudio la moyoni na kwenye fikra kwamba anaondosha Hadathi. Nia ni sharti katika ibada zote, kama Mtume, swallalahu alayhi wasalam, alivyosema kwamba: «Hakuna vingine isipokuwa kwamba ibada ni kwa nia». (Bukhari, Hadithi Na. 1. Muslim, Hadithi Na. 1907). Halafu ataanza kutawadha kwa mpangilio ufuatao, akifuatisha bila ya kuwepo kusita kurefu baina vitendo vya Udhu:

1

Atasema: Bismi-laah (Kwa jina la Allah).



2

Ataosha viganja vyake kwa maji mara tatu au mara mbili au mara moja zote ni sunna.



3



Atasukutua kwa maji; kwa maana ya kuingiza maji mdomoni mwake, kuyatikisa yakiwa ndani halafu kuyatema. Inapendekezwa kwake kufanya hivyo mara tatu.

4

Atafanya Istinshaaq kwa maana ya kuyavuta maji puani mwake halafu kuyatoa kwa kupumua; yaani kuyatoa maji nje kwa hewa itokayo puani. Inapendekezwa kwake kuyafikisha ndani zaidi maji isipokuwa tu kama kufanya hivyo kutamletea madhara. Inapendekezwa kwake kurudia hivyo mara tatu.



**Ataosha uso wake.** Uso ni kuanzia juu ya paji kwenye maoteo ya nwele mpaka chini ya kidevu. Na kutoka sikio mpaka sikio. Masikio sio sehemu ya uso. Inapendekezwa kwake kufanya hivyo mara tatu. Wajibu ni mara moja.







Ataosha mikono yake kuanzia ncha za vidole vyake mpaka kwenye kongo. Kongo zinaingia katika kuoshwa. Inapendekezwa kwake kurudia mara tatu. Wajibu ni mara moja.

Atapaka maji kichwa chake kwa kuilowesha maji mikono yake, halafu apake kichwa chake kwa kuanzia mbele ya kichwa mpaka mwisho wa kichwa kwa upande wa kichogo. Ni sunna kwake kuirudisha mikono huku akipaka mpaka sehemu ya mbele ya kichwa, mara nyingine. Haipendekezwi kwake kurudia kufanya hivyo mara tatu kama ilivyo kwa viungo vingine.







Atapaka maji masikio yake, kwa kuingiza vidole vyake vya shahada katika masikio yake baada ya kupaka maji kichwa chake, na kupaka sehemu ya nje ya masikio yake kwa kutumia vidole gumba.

Ataosha miguu yake pamoja na nguvu. Inapendekezwa kurudia hivyo mara tatu. Wajibu ni mara moja. Ikiwa mtu amevaa soksi, inafaa kwake kupaka maji juu yake kwa shuruti. (Tazama uk. 97).



## Hadathi kubwa na kuoga

### Yanayowajibisha kuoga:

Hayo ni mambo ambayo Muislamu akiyafanya itamlazimu kuoga kabla ya kusali na kutufu. Kabla ya kuoga kwake, anapewa wasifu kwamba ana Hadathi Kubwa.

**Mambo haya ni kama ifuatavyo:**

1 **Kutokwa na manii kwa kuruka kwa matamanio,** na kwa kutumia kitu chochote, na katika hali zote; akiwa macho au usingizini.

Manii ni kimiminiko cheupe, kizito ambacho kinatoka wakati kilele cha matamanio na burudani.

2 **Kujamiiana.** Makusudio ni kuingiza sehemu ya siri ya mwanaume katika sehemu ya siri ya mwanamke, japo litafanyika hilo bila ya kutoa manii. Inatosha katika kuwajibika kuoga kuingiza kichwa cha sehemu ya siri ya mwanaume. Allah Mtukufu amesema kuwa: «Na mkiwa na Janaba, jitwaharisheni». (Sura Almaaida, aya 6).

3 **Kutoka kwa damu ya Hedhi na Nifasi:**

Hedhi ni damu ya maumbile ambayo humtoka mwanamke kila mwezi. Kwa kawaida huendelea kutoka kwa siku saba; zinaweza kuzidi au kupungua kwa kutegemea tofauti ya maumbile ya wanawake.

Nifasi ni damu inayomtoka mwanamke kwa sababu ya kuzaa kwake, na inaweza kuendelea kutoka kwa siku kadhaa.

Mwanamke mwenye Hedhi na mwenye Nifasi anapata tahfifu wakati wa kipindi cha kutokwa na damu. Inamuondokea swala na funga. Atalipa funga na hatalipa swala baada ya kutwaharika kwake. Na haifai kwa mumewe kujamiiana naye katika kipindi hicho, na lakini inafaa kustarehe kwa namna ilio chini ya hapo. Inamlazimu kuoga wakati wa kukatika kwa damu.

Allah Mtukufu amesema kuwa: «basi waepukeni wanawake katika Hedhi, na msiwasogelee mpaka watwaharike. Wakitwaharika, waendeeni katika namna alivyokuamrisheni Allah». (Sura Albaqara, aya 222). Maana ya «wakitwaharika» ni wakishaoga.



**Inamlazimu Muislamu ikimpata Hadathi Kubwa kuoga. Kuoga kunapatikana kwa kueneza mwili wake wote kwa kutumia maji yaliyo Twahara kwa namna yoyote.**

## Muislamu atajitwaharisha vipi janaba au hadathi kubwa?

- Inamtosha Muislamu kukusudia kujitwaharisha kuumwagia maji mwili wake wote.
- Lakini jambo kamili zaidi ni kustanji kama anavyofanya baada ya kwenda haja. Halafu atatawadha. Halafu ataumwagia maji mwili wake. Hilo litazifanya kuwa kubwa zaidi thawabu zake, kwa kuwa amefuata sunna ya Mtume, swallalahu alayhi wasalam.
- Muislamu akioga kwa ajili ya Janaba itamtosha na hahitaji kutawadha, na pia halazimiki kutawadha pamoja na kuoga. Lakini jambo bora zaidi ni kuoga kunakojumuisha kutawadha, kama ilivyo Sunna ya Mtume, swallalahu alayhi wasalam.

## Hali maaalum katika twahara

### Kupaka maji juu ya soksi:

Ni katika wepesi wa Uislamu kwamba Muislamu, kwa kutumia mkono wake ulioloweshwa kwa maji, anaweza kupaka sehemu ya juu ya soksi zake au kiatu chake kilichofinika mguu wote, badala ya kuosha mguu wake katika kutawadha, kwa sharti kwamba awe amevaa soksi au kiatu hicho akiwa na Udhu. Upakaji maji huo unadumu kwa muda usiozidi saa 24 kwa mkazi, na saa 72 kwa msafiri.

Ama katika kuoga kwa ajili ya Janaba, ni wajibu kuiosha miguu katika hali zote.

### Kupaka maji juu ya  kichacha:

Kichacha ni kitu kinachowekwa juu ya viungo vya Udhu wakati wa kuvunjika au kupata jeraha ili kisaidie katika kupona haraka na kupunguza maumivu. Katika kichacha, yanasisitizwa mambo yafuatayo:

- Kwa kutumia mkono ulioloweshwa kwa maji inatosha kupaka juu ya kichacha wakati wa kuhitaji kichacha hicho; sawa iwe katika kutawadha au kuoga kwa ajili ya Janaba.
- Ni wajibu kwake kuosha sehemu iliyo wazi katika kiungo, na kuipaka kwa mkono wake ulioloweshwa kwa maji sehemu iliyofinikwa na kichacha.
- Ataendelea kupaka maji juu ya kichacha, hata kama muda utakuwa mrefu, madamu anakihitaji kichacha hicho. Ni wajibu kwake kukiondosha kichacha pale tu haja itakapokwi**sha**



Sheria inaruhusu kupaka maji viatu na soksi wakati wa kutawadha iwapo Muislamu amevaa viatu au soksi hizo akiwa katika Twahara.

## Mtu aliyeshindwa kutumia maji:

Muislamu akishindwa kutumia maji katika kutawadha au kuoga kwa sababu ya ugonjwa au kwa kuyakosa maji au kwamba maji yapo ila tu hayatoshi isipokuwa kwa kumnywa tu, sheria inamtaka kutayamamu kwa kutumia mchanga, mpaka apate maje na aweze kuyatumia.



## Namna ya kutayamamu:

Ni kupiga mikono yake juu ya mchanga, pigo moja. Halafu kwa kutumia mchanga uliobaki mkononi, atapaka uso wake. Halafu atapaka sehemu ya nje ya kiganja chake cha kulia kwa kutumia kiganja chake cha kushoto, na kinyume chake. Imethibiti katika mafundisho ya Mtume (Sunna) namna nyingine. Namna hiyo ni kupiga mchanga pigo la pili baada ya kupaka uso wake. Halafu atapaka mikono yake mpaka kwenye fundo mbili.



# Kanuni za maumbile

## Ni nini makusudio ya kanuni za maumbile?

Kanuni za maumbile ni mambo ambayo Allah amewaumba wanadamu wawe nayo, na ambayo Muislamu kwa kuyafanya anakuwa mkamilifu, na kwa sababu hiyo, anakuwa katika sifa nzuri sana na muonekano mzuri sana. Hiyo ni kwa sababu Uislamu umezingatia maeneo ya uzuri na umaridadi kwa Muislamu ili awe na wema wa nje pamoja na wema wa ndani.

Mtume, swallalahu alayhi wasalam, amesema kuwa: «Maumbile ni mambo matano: Kutahiri, kunyoa nywele za sehemu za siri, kupunguza sharubu, kukata kucha na kunyoa nywele za kwapa». (Bukhariy, Hadithi Na. 5552. Muslim, Hadithi Na. 257).

**Kutahiri:** Ni kuondoa ngozi ya sehemu ya mbele ya uume (gozi). Kwa kawaida hilo linafanyika katika siku za mwanzo za kuzaliwa.

Jambo hilo ni miongoni mwa mambo yanayopendekezwa na kusisitizwa sana, na ni miongoni mwa kanuni za maumbile kwa mwanamume, na ni jambo lenye faida nyingi za kiafya.

**Kunyoa nywele za sehemu za siri:** Ni kuondoa nywele ngumu kwenye kinena kwa kuzinyoa au kwa njia nyingine yoyote.

**Kupunguza sharubu:** Kuziacha sharubu ni mambo yaliyoruhusiwa, na si jambo linalopendekezwa. Lakini Muislamu akiziacha, ni wajibu kwake kutoziacha zikawa ndefu sana. Anatakiwa azitunze kwa kuzipunguza.

**Kufuga ndevu:** Uislamu unahimiza kufuga ndevu ambazo ni nywele zinazo ota kwenye taya,mashavu na kidevu.

Maana ya kuzifuga ni kuziacha na kutozinyoa, ikiwa ni kuiga Sunna ya Mtume, swallalahu alayhi wasalam.

**Kukata kucha:** Inatakiwa kwa Muislamu kuzipatiliza kucha zake kwa kuzipunguza ili zisiwe mahali pa taka na uchafu.

**Kunyonyoa kwapa:** Inatakiwa kwa Muislamu kuondoa nywele za kwapa kwa kuzitoa kwa mkono au kwa kitu kingine chochote kinacho ondosha, ili kuzuia asitokwe na harufu mbaya.

